# TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# TAARIFA YA KAIMU MKURUGENZI, DKT. K.A. NIHUKA ILIYOTOLEWA KWENYE MKUTANO WA WAFANYAKAZI – MAKAO MAKUU, DAR ES SALAAM TAREHE 27/06/2018

**JUNI, 2018**

***Kaimu Naibu Mkurugenzi Mipango, Fedha na Utawala,***
***Kaimu Naibu Mkurugenzi Taaluma, Utafiti na Ushauri,***
***Mwenyekiti THTU na RAAWU,***
***Wakuu wa Idara na Vitengo,***
***Wafanyakazi wenzangu,***
***Mabibi na Mabwana,***

Awali ya yote tunamshukuru Mungu kwa kutufikisha katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2017/2018 salama. Nitumie nafasi hii pia kuwapongeza wafanyakazi wote wa Makao Makuu – Dar es Salaam na Vituo vya Mikoa yote Tanzania bara kwa kuendelea kufanyakazi kwa bidi na maarifa na kuifanya Taasisi yetu iendelee kusonga mbele. Wakati tukijipanga kuanza mwaka mpya wa fedha 2018/2019, tumeitisha mkutano huu wa wafanyakazi ili tupeane taarifa ya mambo muhimu yaliyotokea katika robo ya nne tunayoimaliza. Taarifa hizi zinatokana na maamuzi mbalimbali yaliyofanywa kwenye vikao vya menejimenti vya kila mwezi pamoja na mkutano wa mwaka wa wakufunzi wakazi na mkutano wa tisa (09) wa Baraza la wafanyakazi.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Katika robo hii ya nne, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria kadiri ya Hati Idhini (Act) Na.12 ya 1975. Kama mnavyofahamu, Bodi ya Usimamizi ya TEWW ilimaliza muda wake tarehe 3.04.2018. kwa sasa, menejimenti inaendelea kuwasiliana na mamlaka husika ili tuweze kupata Bodi ya Usimamizi na tutaendelea kuwajulisha kadiri tunavyopata taarifa. Ni matarajio ya menejimenti kuwa tutaingia robo ya kwanza ya mwaka mpya wa fedha wa 2018/2019 tukiwa na Bodi. Pia, TEWW inakamilisha andiko la “Annual Activity Report” na “Facts and Figures” ya TEWW ya mwaka 2018. Timu mbili ziliundwa ili kufanya kazi hii ambapo menejimenti ili mteua Bw. Patrick Kisigiro kuwa Mwenyekiti wa timu ya kuandika “Annual Activity Report” na Bw. Celestine Magesa kuwa Mwenyekiti wa timu ya kuandika “Facts and Figures”. Wajumbe wengine walikuwa ni Justine Mbwambo, Sylvester Mbumbe, Elianaike Marti na Neema Rumisho. Wengine ni Mwajuma Mohamedi, Samweli Gasuku, Shaban Maijo na Leticia Kulekana. Kazi hii ilifanyika ADEM Bagamoyo na rasimu ya awali

ya nyaraka zote mbili imewasilishwa kwa Mkurugenzi kupitia kwa AMTA kabla ya kuzikamilisha, kuzichapa na kuzisambaza kwa wadau mbalimbali.

Kwa niaba yenu na ya menejimenti, nawashukuru sana wenyeviti wa timu zote mbili pamoja na wote walioshiriki pamoja na ofisi ya AMU na AMTA kwa uratibu wa kazi hii.

***Wafanyakazi wenzangu***,

Katika kipindi cha robo ya nne ya 2017/2018, TEWW imeanza kazi ya kudurusu Mpango Mkakati wa Taasisi (Rolling Strategic Plan – RSP) ambao muda wake utafikia ukomo mwezi Julai, 2019. Timu iliyoundwa kufanya kazi hii, inayoongozwa na Afisa Mipango na Maendeleo, Fidrish Fredson imekamilisha na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi kupitia ofisi ya AMU taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa sasa kabla ya kuendelea na hatua inayofuata. Wajumbe wengine wanaofanya kazi hii ni Dkt. Sempeho Siafu, Dkt. Godfrey Mnubi, Bi. Mary Kimaty na Bi. Janeth Nsenga. Ni matarajio ya menejimenti kuwa mkakati mpya utapatikana kwa wakati ili uanze kutumika kuanzia tarehe 01. Julai, 2019.

Kwa niaba yenu na ya menejimenti, nawashukuru wote kwa kufanya kazi hii ya awali kwa umakini mkubwa.

Aidha, ili kutekeleza RSP ya sasa kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2018/2019, ofisi ya AMU kwa kushirikiana na Utumishi wamepanga kukamilisha ujazaji fomu za OPRAS kwa mwaka 2018/2019 kabla ya tarehe 15.07.2018 sambamba na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wote. Kwa sasa, tathmini ya mwaka ya utekelezaji wa OPRAS za mwaka 2017/2018 inaendelea na itakamilika tarehe 29.06.2018. Hivyo, nitumie nafasi hii kumhimiza kila mmoja wetu kukamilisha kujaza fomu za tathmini ya mwaka ya utekelezaji wa OPRAS kwa mwaka 2017/2018 na kujaza OPRAS kwa ajili ya mwaka 2018/2019.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Kama mnavyofahamu, moja ya maeneo ya kipaumbele ya TEWW kwenye RSP ni kuifanya TEWW iweze kujitegemea kimapato katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria. Ninapenda kuwafahamisha kuwa ili kutekeleza hili, TEWW imeanza kutekeleza mkakati wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima kwa kuelekeza matumizi kwenye maeneo ya kipaumbele ya TEWW, Idara na Vituo vya Mikoa kuanzia robo hii ya nne. Kupitia mkakati huu, wamiliki wa "Open Schools" wameagizwa kulipa ada za uratibu kwa wakati pamoja na kuzingatia vigezo vya usajili wao ikiwemo kulipa michango ya mitihani ya utamilifu. Pia, wanafunzi wetu wote wa elimu ya juu katika vituo vya mikoa na Kampasi zote wamehimizwa kulipa ada kadiri ya miongozo ya TEWW inayowataka kulipa 50% muhula wa kwanza na 50% muhula wa pili na zilipwe kabla ya mitihani kuanza. Kuhusu matumizi ya vituo, kuna malipo yatakayo kuwa yanatumwa moja kwa moja kwa watoa huduma na yale yatakayokuwa yanatumwa vituoni kwa matumizi ya vituo. Aidha utekelezaji wa programu ya elimu ya sekondari utaratibiwa na Idara ya Elimu Masafa kupitia Idara ya Uratibu Vituo Mikoani kwa maana ya kuandaa bajeti na kuratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Sambamba na kuimarisha makusanyo ya mapato ya TEWW, makao makuu na Kampas zetu za Luchelele – Mwanza na WAMO – Morogoro vitaanza kutumia GePG katika kukusanya mapato ya TEWW kuanzia Julai mosi, 2018. Aidha, vituo vya mikoa vitaanza kutumia mfumo huu kadiri wanavyowezeshwa kupata vitendea kazi kama Kompyuta na "Internet".

***Wafanyakazi wenzangu,***

Katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2017/2018, TEWW imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hapa makao makuu na baadhi ya vituo vya mikoa. Katika kituo cha Mkoa wa Kilimanjaro, tumekamilisha hatua ya kwanza ya ukarabati wa darasa moja na awamu ya pili itaanza mapema mwezi Julai. Aidha, tumekamilisha michoro na gharama za kufanya upanuzi wa maktaba makao makuu – Dar es salaam, pavementi za maeneo ya nje ya vyumba viwili

vipya vya mihadhara na ukarabati wa vyumba vya zamani vya madarasa (vile vidogo vidogo) WAMO – Morogoro pamoja na kuweka viyoyozi. Kazi hizi zitaanza mara baada ya wanafunzi kumaliza mitihani na kwenda likizo. Pia makadirio ya kukarabati vyoo vya walimu na wanafunzi kituo cha WAMO – sekondari Morogoro na madarasa mawili kituo cha Ruvuma na ofisi ya TEWW Mkoani Rukwa yanaandaliwa. Lengo ni kukarabati majengo ya vituo vyote vya TEWW vyenye majengo yake ya kudumu kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu. Vilevile, katika robo hii ya nne, TEWW imekamilisha kuweka samani katika ofisi ya Msajili, ofisi ya EKU na ofisi ya utafiti kwa hatua ya kwanza. Pia, tumeweka taa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya mwanga na kuimarisha usalama. Lengo ni kuhakikisha ofisi zote zenye mahitaji zinafikiwa.

Shughuli nyingine ya maendeleo iliyofanyika ndani ya robo ya nne ni kuweka Mtandao wa Internet (LAN) hapa makao makuu. Katika kipindi hiki, TEWW imekamilisha kazi ya kuweka LAN katika jengo la makao makuu kwa kutumia wataalamu wa TERNET kwa gharama nafuu. Aidha, tutawatuma wataalamu wa TERNET waende Kampasi ya WAMO na Luchelele ili wakatathimini mahitaji na gharama za kuweka LAN katika Kampasi hizo ili kuweza kuwawekea LAN ili kurahisisha mawasiliano na ufundishaji na ujifunzaji katika Kampasi zetu.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Katika robo hii ya nne, tumefanikiwa kuanza kutekeleza kazi ya kuthaminisha rasilimali za TEWW zikiwemo viwanja na majengo yote ya makao makuu na vituo vya mikoa. Kazi hii ambayo imeanza tarehe 26.06.2018 inafanywa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu Ardhi na itakamilika baada ya wiki tatu kwa gharama ya shilingi 35,000,000/= ambapo malipo ya awali ya shilingi 10,000,000/= yameshafanyika na kazi inaendelea.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Masuala ya kitaaluma yaliendelea kutekelezwa kama kawaida katika Kampasi ya Dar es salaam, WAMO – Morogoro na Luchelele pamoja na vituo vyote vinavyoendesha mafunzo ya Diploma (ODL). Pamoja na hiyo, udurusu wa mitaala ya mafunzo unaendelea kupitia Idara ya Mafunzo. Taarifa zinaonesha kuwa hadi sasa kazi hiyo ipo katika hatua nzuri. Lengo la udurusu ni kuhuisha mitaala yetu ili iendane na mahitaji halisi ya sasa.

Vile vile napenda kuwafahamisha kuwa, mitihani ya mwisho wa muhula wa pili kwa mwaka 2018 imeanza leo tarehe 27 Juni, 2018 katika Kampasi ya Dar es salaam, WAMO – Morogoro na Luchelele – Mwanza kwa wanafunzi wanaosoma kwa njia ya kawaida (regular mode). Kwa upande wa wanafunzi wanaosoma kwa njia huria na masafa (ODL), mitihani yao ilianza tarehe 11. Juni, 2018 katika vituo vyote 33 (yaani vya mikoa 17 na wilaya 16) na imekwisha salama.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Katika kuunga mkono juhudi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuinua stadi za kisomo nchini, TEWW imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Kuinua Kisomo na Elimu kwa Umma katika kipindi hiki cha robo ya nne ambao utaanza kutekelezwa kuanzia Julai, 2018 katika mikoa ya Tanzania bara kwa kutumia wanafunzi wetu wa Astashahada, Stashahada na Shahada na wadau wengine wanaopenda kuungana na TEWW yakiwemo mashirika ya dini, mashirika yasiyo ya kiserikali na watu binafsi. Ni matarajio ya menejimenti kuwa Ofisi ya AMTA itahakikisha kuwa "typesetting" na uchapaji / uzalishaji wa nakala ngumu za mkakati huo vinakamilika na uzinduzi unafanyika mwezi Julai, 2018. Kwa sasa, utafiti mdogo unafanywa na kitengo cha Utafiti, Machapisho na Ushauri chini ya usimamizi wa Dkt. Godfrey Mnubi ili kujifunza uendeshaji wa kituo cha kisomo cha Chamwino Dodoma. Uzoefu huu utatusaidia katika kutekeleza vituo vya kisomo nchi nzima.

***Wafanyakazi wenzangu,***

Kuhusiana na masuala ya wafanyakazi, napenda niwajulishe yafuatayo; mosi, utaratibu wa kumpata uteuzi wa Naibu Mkurugenzi (Mipango, Fedha na Utawala), unaendelea vizuri na upo katika hatua ya upekuzi (vetting). Hivyo kwa sasa, Bi. Mary Watugulu anaendelea kukaimu katika nafasi hiyo.

Kuhusu waliopata utwalii, katika kipindi cha robo ya nne, wafanyakazi 44 wamepandishwa daraja / cheo na mishahara yao kuongezeka:

Aidha, wafanyakazi 5 wamepandishwa daraja / cheo bila kuongezewa mishahara kwa sababu mishahara yao ya sasa inaendana na kiwango walichofikia.

Hata hivyo wapo Watumishi wawili ambao hawajapanda daraja / cheo hawajabadilishiwa mshahara kutokana na ufaulu wa Shahada zao kuwa chini ya 3.5 kulingana na vigezo vya NACTE.

***Wafanyakazi Wenzangu,***

Napenda pia kuwajulisha kuwa, kutokana na uhaba na uchakavu wa magari ya Taasisi, menejimenti imeamua kuwa manaibu wakurugenzi wote wawili (AMU na AMTA) watapewa fedha ya mafuta ya gari kwa ajili ya usafiri wa kutoka nyumbani kuja ofisini na kurudi nyumbani kama inavyofanyika kwenye Taasisi nyingine za Serikali. Aidha gari aina ya Nissan limetengenezwa na limepelekwa kituo cha Mkoa, Iringa tarehe 10.06.2018 kwa ajili ya matumizi ya kituo.

***Wafanyakazi Wenzangu,***

Kuhusu maendeleo ya wafanyakazi kitaaluma, Taasisi imeendelea kutoa fursa kwa wafanyakazi kujiendeleza katika fani zao. Hata hivyo, katika robo ya nne, Taasisi kupitia ofisi ya Afisa Sheria inapitia mkataba wa kuwasomesha wanataaluma ambapo taasisi huwa ni mlipaji wa pesa zote alizokopeshwa mtumishi na HESLB ili kugharamia masomo yake ili uendane na hali halisi ya sasa

ambapo mtumishi atawajibika kufanya marejesho ya mkopo aliochukua HESLB. mara tu amalizapo masomo yake.

Nitumie nafasi hii kuwahimiza wote walioko masomoni kwa ngazi mbalimbali kuhakikisha wanamaliza masomo yao kwa wakati ili warudi kuijenga Taasisi yetu na Taifa kwa ujumla.

Mwisho, napenda kuwashukuru sana manaibu wakurugenzi wote wawili, wakuu wa Idara na Vitengo na wafanyakazi wote kwa ujumla kwa ushirikiano mnaonionesha katika utekelezaji wa majukumu ya ofisi ya Mkurugenzi. Ni matumaini yangu kuwa tataendeleza ushirikiano, umoja, upendo na amani iliyopo ili kwa pamoja tuweze kufikia dhamira ya taasisi ya kujenga jamii iliyoelimika na inayojiendeleza kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**Mungu Ibariki TEWW**

**Mungu Ibariki Tanzania**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**